# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

AFISA MTENDAJI ,
KIJIJI CHA NANGA,
S.L.P 19,
IGUNGA.

18.07/2022.

**<u>YAH: HATI YA UTAMBULISHO WA ENEO LA KAMPUNI TA TAUR TANZANIA LIMITED LENYE UKUBWA WA EKARI 10.6.</u>**

Husika na somo tajwa hapo juu,

Kwaniaba ya Halmashauri ya kijiji cha Nanga napenda kulitambulisha eneo lenye urefu wa mita **251** na upana wa mita **171** ambalo upande wa mashariki limepakana na shule ya sekondari Nanga,magharibi limepakana na Dotto siningi ,kusini limepakana na mzee Haruna ,upande wa kaskazini limepakana na ndugu Kishiwa malendeja , kwamba eneo hilo ni mali halali na linamilikiwa na kampuni ya TAUR TANZANIA LIMITED ambalo walilinunua kwa Ndugu Kishiwa Malendeja tarehe 08/09/2011 . kwa mauziano halali ya kiserikali.

SAHIHI YA MWENYEKITI

..........................................

ATANASI K. DAUDI

HALMASHAURI YA KIJIJI CHA NANGA
REG TBR/IAC/Nº 309
TAREHE 18/0/22
IGUNGA

SAHIHI YA KATIBU

..........................

HENERY L. MASANJA

AFISA MTENDAJI
KIJIJI CHA NANGA
IGUNGA

# HALIMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

# KIJIJI CHA NANGA

M /KITI WA KITONGOJI CHA MBUYUNI

S.L.P 108

NANGA IGUNGA

TAREHE 05/07/2022

Certified as a True Copy of the Original
Date: 13/07/2022 Sign: ...........
FADHIL R. KINGU
Advocate Notary Public &
Commissioner for Oaths

## YAH: HATI YA KUUZIANA ENEO.

Mimi ..Kishiwa Malendeja Kushiwa..mkazi wa ..........Nanga..........kitongoji cha ......Mbuyuni.......... Nakili kuuza ......Eneo........ kwa ndugu.Jamb Tanzania Ltd mkazi wa kitongoji cha ......Nanga..........kwa thamani ya Tsh:...6,000,000......(......Milioni Sita tu..........)kuanzia leo tarehe ...6/7/2022 mmiliki halali wa eneo hili ni Jamb Tanzania Limited........

kinyume/lolote litakalojitokeza kubaini udanganyifu mkono wa sheria uchukue mkondo wake.

urefu wake ni . .Mita 251.........na upana wake ni ..Mita 171..............Mashariki kimepakana na..Sekondari..........magharibi kimepakana na Doto Simong'i...
kusini kimepakana na mzee Haruna..na kaskazini kimepakana na mzee Kishiwa Malendeja



PICHA YA MUUZAJI

PICHA YA MNUNUZI



SIMU NA: 0752 355183 ...
JINA LA MUUZAJI..Kishiwa Malendeja
SAHIHI YA MUUZAJI Kishiwa..............

SIMU NA..0757729971........
JINA LA MNUNUZI...Jamb Tanzania Limited
SAHIHI YA MNUNUZI..........................
Kwa niaba ya Kampuni

HIZI NI SAHIHI ZA MASHAHIDI WALIOSHUHUDIA MAKUBALIANO HAYA

**Mashahidi muuzaji**

1.Jina..Kushiwa Mahembe....Sahihi Kushiwa...

2.Jina.....Athanus Daudi......Sahihi..............

1.Jina Onesimu Gerald sahihi.............

**Mashahidi wa mnunuzi.**

1.Jina Musa Pascal sahihi..............

2.Jina..Emith Moses sahihi..............

2.Jina..Doto Simong'i sahihi..............

Mauziano haya yamefanyika mbele
Yangu..Jonas Livingstone..........
Sahihi.................................
Tarehe 06/07/2022.............

Mwenyekiti wa Kitongoji Mbuyuni Kijiji cha Nanga 06/07/2022

Scanned with CamScanner

# MKATABA WA KUUZA KIWANJA

MKATABA HUU umesainiwa leo tarehe ...06... Mwezi ...July..... 20.22...

**KATI YA**

**KISHIWA MALENDEJA KISHIWA,** wa S.L.P [0784-166865], Nanga- Igunga, Tabora (Baada ya hapa atatajwa kama "**Muuzaji**") neno ambalo litamjumlisha yeye, wakala wake na warithi wake) kwa upande mmoja;

**NA**

**TAUR TANZANIA LIMITED** kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za makampuni Tanzania, ya S. L. P 123, **IGUNGA-TABORA** (Baada ya hapa atatajwa kama "**Mnunuzi**") neno ambalo litamjumlisha yeye, wakala wake) kwa upande mwingine

**KWA MKATABA** huu, **Muuzaji** ambaye ni Mmiliki halali wa Kiwanja ambacho hakijapimwa kilichopo katika Kitongoji cha Mbuyuni, kijiji cha Nanga, Wilaya ya Igunga Mkoa wa Tabora, chenye ukubwa wa ekari........10.6................ kwa malipo ya **fedha Shilingi Milioni Sita (Tshs.6,000,000/=)tu** anakubali kwa hiari yake mwenyewe kumuuzia **Mnunuzi** kiwanja hicho.

**NA KWA KUWA MKE WA MUUZAJI** (Bi MAGDALENA SETEPOEHO........) ambaye ametia saini kama shahidi wa mkataba huu, ameridhia uuzwaji wa kiwanja hicho, MNUNUZI anaamua kuinunua ikiwa haina pingamizi lolote toka kwa mke wa muuzaji.

**MIPAKA YA KIWANJA**

i) Kaskazini kimepakana na eneo la ..MZEE KUHWA MALENDEJA.
ii) Kusini kimepakana na .....MZEE HARUNA....................
iii) Mashariki kimepakana na .SEKONDARI............................
iv) Magharibi kimepakana na ...NATO SINIBHI..................

**KWA MKATABA HUU** Muuzaji na Mnunuzi wanakubaliana kama ifuatavyo kwamba;

i) Muuzaji anakiri kupokea malipo ya fedha **Taslimu za Kitanzania Shilingi Milioni Sita (Tshs 6,000,000/=)** Fedha hizo zimelipwa kwa mkupuo mmoja kabla ya tarehe ya kusaini mkataba huu. Fedha hizo zitatambulika kwenye mkataba kama fedha za kununua kiwanja.

ii) Fedha zote zimelipwa taslimu/mkononi mwa Muuzaji wakati wa kusaini mkataba huu mbele ya mashahidi wanaonekana kwa majina yao kwenye mkataba huu.

iii) Muuzaji anathibitisha kwamba kiwanja anachokiuza pamoja na vitu vyote vilivyoshikamana na ardhi, ni mali yake binafsi na hakuna mtu, watu, taasisi au kikundi chochote chenye madai ya aina yoyote ile yenye kuhusisha na kiwanja tajwa hapa

iv) Muuzaji anahamisha umiliki wa kiwanja kilichotajwa kwenye mkataba huu kwa Mnunuzi bila masharti mengine kando na haya yaliyotajwa katika mkataba huu.

v) Ikiwa kutatokea matatizo yoyote katika kuhamisha umiliki wa kiwanja tajwa/ husika, Muuzaji anakubali kurejesha fedha zote alizopokea kama malipo ya uuzaji wa kiwanja tajwa katika mkataba huu.

vi) Baada ya malipo yaliyofanyika leo siku ya kusaini mkataba, Muuzaji atamkabidhi Mnunuzi kiwanja pamoja na hati miliki ya ardhi, leseni ya makazi

Certified as a True Copy of the Original
Date: 8/07/2022 Sign: [signature]
FADHIL R. KINGU
Advocate Notary Public &
Commissioner for Oaths

Scanned with CamScanner

na/au nyaraka yoyote inayoonyesha umiliki wa kiwanja tajwa, na Mnunuzi ameshamkabidhi Muuzaji fedha taslimu ya manunuzi ya kiwanja

vii) Mnunuzi kwa gharama zake mwenyewe na kwa kuzingatia taratibu, kanuni na sheria za ardhi, atagharamikia gharama za kupima/ kubadili jina la muuzaji kwenda kwenye jina lake.

viii) Kwamba mkataba huu ni muendelezo wa makubaliano ya tarehe 08/09/2011, kuwa mkataba huu utawekwa kwenye maandishi baada ya upimaji wa kiwanjwa tajwa kwenye mkataba huu kukamilika.

ix) Kwamba kuungua,kuchanika au kupotea kwa mkataba huu kamwe hautomaanisha makubaliano baina ya Muuzaji na Mnunuzi yamevunjika.

x) Kwamba kwa kusaini mkataba huu pande zote mbili zinathibitisha na kukubali kuwa tatizo lolote litakalotokea katika mkataba huu litatatuliwa katika Mahakama zilizo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mkataba huu utatafsiriwa na kulindwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**IMESAINIWA** na **KISHIWA MALENDEJA KISHIWA** ambaye namfahamu / ametambulishwa kwangu na KISHIWA ... MALENDEJA ..ambaye namfahamu Mbele yangu leo hii tarehe ..06. mwezi ..July.., 20.22.

KISHIWA

**MUUZAJI**

**SHAHIDI WA MUUZAJI**

| **JINA** | **SAINI** |
|---|---|
| 1. MAGRENA · STEPHANO (Mke wa Muuzaji) | M· S |

**IMESAINIWA** na **MARTIN DEOGRATIAS GEORGE** Kwaniaba ya TAUR TANZANIA LIMITED ambaye namfahamu /ametambulishwa kwangu na.................... ambaye namfahamu mbele yangu leo hii tarehe...06..... mwezi ...July......, 20...22...

**MNUNUZI**

**SHAHIDI WA MNUNUZI**

| **JINA** | **SAINI** |
|---|---|
| 1. MUSA PASCHAL | [signature] |

**MBELE YANGU:-**

**JINA:** JOHNI-LIVINGISTONE

**SAINI:** [signature]

**ANWANI:** 0755739063

**NAFASI/CHEO:** M/KITONGOJI

MWENYEKITI WA KITONGOJI MBUYUNI KIJIJI CHA [illegible] 06/07/2022



Scanned with CamScanner